

Tanzania

# Kuongeza Sifa za Kuajiriwa kwa kupitia Mafunzo ya Ufundi Stadi (EEVT)

Mradi wa VETA, VSO na BG Tanzania
Juni 2012 – Mei 2015

VSO

VETA

BG TANZANIA

Mradi wa EEVT (Kuongeza Sifa za Kuajiriwa kupita Mafunzo ya Ufund Stadi) unatekelezwa na Mamlaka ya Elimu ya Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) na shirika la maendeleo la kimataifa la VSO, kwa kushirikiana na BG Tanzania. Mradi wa EEVT una lengo la kuboresha ajira kwa vijana katika mikoa ya Mtwara na Lindi Kusini mwa Tanzania, kwa kuzingata ongezeko la mahitaji ya wafanyakazi wenye ujuzi katika sekta ya gesi na huduma zinazohusiana nayo. Kwa zaidi ya miaka 2, walimu wa VETA na wanafunzi wao watapewa mafunzo na wakufunzi kutoka VSO. Hatimaye, VETA itakuwa na uwezo wa kutoa kundi imara la mafundi na walimu wenye vigezo.

## Kwa nini? – Hiitaji la stadi za ufundi katika mikoa ya Mtwara na Lindi

Kutokana na ongezeko kubwa katika shughuli za uvumbuzi unaofanywa na makampuni mbalimbali ya gesi katika eneo hilo, mahitaji ya wafanyakazi wenye ujuzi yameongezeka. Wakati idadi ya wafanyakazi inayohitajika kwa ajili ya shughuli za gesi moja kwa moja ni ndogo, matokeo ya mwenendo wa upatikanaji wa ajira katika mikoa hii yanatarajiwa kuwa makubwa.

## Nini? – Malengo Makuu ya Mradi wa EEVT

VETA Kanda ya Kusini Mashariki hunyanyua viwango vya stadi za ufundi kulingana na viwango vinavyotambuliwa kimataifa katika maeneo ya kitaalamu sita (maandalizi ya chakula, ufundi mabomba, uchome leaji (welding), useremara, ufundi magari, ufungaji umeme), pamoja na maeneo ya jumla kama lugha ya Kiingereza, afya na usalama, matengenezo na ujasiriamali. Walimu wa VETA katika mikoa ya Mtwara na Lindi wanapata mafunzo ya kufundisha wanafunzi kwa mujibu wa viwango vya kimataifa. Msaada kwa walimu ni wa aina mbili: mafunzo ya kila siku ya ujuzi toka kwa wakufunzi wa VSO, na uboreshaji wa sifa kupita mafunzo kadhaa toka kwa City & Guilds (C&G). Kwa zaidi ya miaka 2, wakufunzi wenye uzoefu wa kujitolea wa ufundi stadi kutoka VSO wamekuwa wakiwafuatilia walimu wa VETA kwa karibu na kuwafundisha kila siku mmoja mmoja katika mikoa ya Mtwara na Lindi. Taasisi ya kimataifa ya mafunzo ya ufundi stadi City & Guilds hutoa mafunzo kwa walimu wa VETA katika Stadi za Kufundishia, afya na Usalama, na katika fani zao maalum; mwishoni walimu hufanya mithani kwaajili ya kupata vyeti vya City & Guilds. Aidha, Britsh Council imeendesha mafunzo ya mwezi mmoja kuboresha viwango vya Kiingereza kwa walimu wote 24 wa VETA Mtwara. Wakufunzi kutoka VSO, pamoja na walimu VETA wakisaidiwa na City & Guilds, hufanya maboresho muhimu katika warsha husika kuelekea viwango vya kimataifa.

Sehemu muhimu ya progamu hii ni kutengeneza muunganiko imara wa kisekta, kuwatambulisha wanafunzi na walimu katika sekta husika kama sehemu ya mafunzo yao, na kuwawezesha kupata ajira baada ya kuhitimu. BG Tanzania huunganisha mtiririko wa ugavi katika sekta ya gesi, hushauri mahitaji ya sekta na kuwezesha upatikanaji wa mafunzo ya kazi, ziara kwa "vituo" vingine vinavyohusiana na sekta na taarifa juu ya sekta. Uhusiano zaidi utatengenezwa na viwanda vya ndani wakati wote wa Programmu.



## Walengwa

Katika muda mfupi, mradi huu unatarajiwa kuwafikia moja kwa moja walengwa wafuatao:

- Walimu 24 wa VETA kupata msaada wa kazi kutoka kwa wakufunzi wa VSO kila siku
- Walimu 11 wa VETA kupata mafunzo kadhaa ya City & Guilds na kufanya mithani ya kupata vyeti vya City & Guilds
- Wanafunzi 620 wa VETA kufaidika na mazingira bora ya elimu, uwepo wa wakufunzi wa VSO, na walimu wa VETA waliothibitshwa
- Wanafunzi 280 wa VETA watapata nafasi zaidi ya kutafuta kazi baada ya kuhitmu.

Hatimaye, walimu teule wa VETA watatoa ujuzi wao kwa wafanyakazi wapya wa VETA, wakiwezesha VETA Kanda ya Afrika ya Mashariki kutoa kundi imara la mafundi na walimu wenye ujuzi. Kwa njia hii, VETA inaunda faida ya pande zote, kwa wenyeji wa Mtwara na kwa ajili ya sekta hii.

## Maeneo Yanayoshughulikiwa

Shughuli sita maalum:

- Maandalizi ya chakula
- Ufundi mabomba na ufungaji mabomba
- Uchomeleaji na uundaji (Welding and Fabricaton)
- Useremala na useremala wa ujenzi wa nyumba
- Ufundi Makanika wa Magari
- Ufungaji Umeme

Pamoja na maeneo ya jumla kama lugha ya kiingereza, afya na usalama, matengenezo na ujasiriamali.

## Washirika Wakuu

- Mradi huu unafanyika VETA Kanda ya Kusini Mashariki, ikihusisha matawi katika mikoa ya Mtwara na Lindi.
- VSO husimamia mradi huu na huleta wakufunzi kufundisha walimu na kuboresha warsha zilizochaguliwa.
- BG Tanzania hufanya kazi kama mfadhili na kiungo kwa sekta ya gesi. City & Guilds husaidia mradi kuelekea katika kutunukiwa vyet vya kimataifa.
- Britsh Council hutoa mafunzo ya Kiingerezakwa vyeti vya kimataifa

## Muda ya mradi

- Tarehe 18 Juni hadi 16 Julai 2012: mafunzo ya Kiingereza na Britsh Council
- Oktoba 2012: kuwasili kwa wakufunzi wa VSO
- Novemba 2012: uzinduzi wa mradi wa EEVT (mgeni wa heshima: makamu wa Rais wa Tanzania)
- 2013: kupanuliwa kwa mradi VETA tawi la Lindi
- Januari 2013 - Desemba 2014: miaka
- miwili ya mafunzo ya walimu na maboresho ya warsha
- Mwishoni mwa 2014: kufuzu viwango vya kimata ifa vya City & Guilds kwa VETA kanda ya kusini mashariki





Kuongeza Sifa za Kuajiriwa kwa kupitia Mafunzo ya Ufundi Stadi Mtwara na Lindi



Mradi wa EEVT ni sehemu ya mradi mkubwa wa VSO wa Riziki Salama, ambao una malengo yafuatayo:

- Taasisi za mafunzo ya ufundi stadi kuongeza viwango vyao kulingana na viwango vinavyotambuliwa kimataifa na mahitaji ya soko.
- Wakulima wadogo wadogo wanapata rasilimali za uzalishaji (ardhi, mikopo midogo), teknolojia sahihi (umwagiliaji, mbegu), utekelezaji wa kilimo kizuri na mahusiano ya soko.
- Mazingira ya kibiashara yanafaa zaidi kwa maendeleo ya sekta binafsi, hasa SME.





Kwa habari zaidi kuhusu mradi huu, tafadhali wasiliana na:
Jean Van Weter, VSO Tanzania Country Director - jean.vanweter@vsoint.org
Rose Tesha, VSO Programme Manager for Secure Livelihoods - rose.tesha@vsoint.org
Wilhard Soko, Regional Director VETA South East Zone - w_soko81@yahoo.com
Joseph Kibehele, Principal VETA Mtwara - jkibehele@yahoo.com
Leonard Malisa, Principal VETA Lindi - leonelimalisa@yahoo.com